# HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA

Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) S.L.P 88, Ngudu

SIMU: 0732980528
Fax: 0732980844
E-mail: dedkwimba@yahoo.com

S.L.P 88,
**NGUDU/KWIMBA.**


Mhe. Mwenyekiti,
Kamati ya Menejimenti ya Halmashauri,
S.L.P 88,
**NGUDU/KWIMBA.**

**YAH :TAARIFA ZA UTEKELEZAJI KWA IDARA NA VITENGO KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.**

## 1.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI IDARA YA MAJI 2016/2017 ROBO YA NNE

**UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA..**

Kwa kipindi cha robo ya nne (April hadi Juni 2017) idara imetekeleza shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:-

| S/No | SHUGHULI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1.0 | Usimamizi wa Ujenzi wa Miradi ya Maji katika Programu ya maji Vijijini, ambapo miradi minane katika Vijiji vya Isunga, Kadashi, Nyanhiga, Igunghya, Igumangobo, Mhande na Izizimba “A” inajengwa | Kazi katika Vijiji vya Igunghya (95%), Nyanhiga (76%) Igumangobo (75%), Isunga (50%), Kadashi (50%), Shilima (45%), Mhande (45%) na Izizimba (35%) |
| 2.0 | Usimamizi wa ujenzi wa Visima kumi unaofadhiriwa na The Desk and Chair katika Kata ya Igongwa kwa kushirikiana na Wananchi. | Ujenzi wa Visima vitano bado havijakamilika na mfadhili haonkani kuendelea na kazi licha ya kutoa ahadi mbalimbali za kurudi eneo la kazi katika Vijiji vya Maguluma (Mnguluma”A”, Sakanti “B” na Mwamala) Kijiji cha Mwadubi na Malemave |
| 3.0 | Kuendelea kuzisaidia Kamati za maji kutatua matatizo ya mitambo na miundo mbinu ya maji wakati matatizo yanapojitokeza | Wataalamu walitoa ushauri na kushiriki malaekebisho ya miundo mbinu ya maji katika Kijiji cha Kiliwi, mantare, Ilumba, Ilula na kwa kushirikiana na Mbunge wa jimbo la Kwimba ukarabati na usafishaji wa visima umefanyika katika vijiji vya Nyanhonge, |

| | | |
|---|---|---|
| | | Milyungu, Buyogo center, Nera secondary, Songe, Buchama, Mwamaya, Kabale, Bugembe, Nyamilama center, Mwaseya, Igongwa, Malemve na Runere |
| 4.0 | Kukusanya na Kuwasilisha takwimu za maji Wizara ya Maji | Taarifa ya hali ya vituo vya maji katika Halmashauri imendaliwa kwa kushirikiana na Watendaji wa Kata na kuwasilishwa Wizara ya Maji |
| 5.0 | Kushiriki katika vikao, na ziara za Viongozi | Idara ilishiriki vikao vya Kisheria ya Halmashauri na ukaguzi wa njia ya mwenge |

**1.0. CHANGAMOTO.**

**1.1.** Upungufu wa vitendea kazi kama pikipiki kwa sasa ni tatizo hadi kupelekea utendaji kazi kuwa mngumu.

**1.2.** Suala la uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji ya bomba unaofanywa na jamii bado ni tatizo hasa katika ukusanyaji wa mapato ya maji na matumizi yake.
,

**1.3.** Suala la utunzaji wa mazingira ambalo ndilo tengemeo kubwa la uwepo wa maji chini ya ardhi, bado ni tatizo.

**1.4.** Utendaji wa Wakandarasi wetu katika miradi ya maji ni wa kiwango cha chini na hawakai maeneo yao ya kazi.

**2.0.** MIKAKATI.

**2.1.** Kuendelea kuikubusha Serikali umuhimu wa kuleta fedha kwa ajili ya uendeshaji wa ofisi na fedha za miradi

**2.2.** Uhamasishaji kwa ajili ya kupanda miti na utunzaji wa vyanzo vya maji uendelee kufanyika

**2.3.** Mafunzo kwa kamati za maji na Jumuia za maji uendelee kufanyika ili kufanya miradi kuwa endelevu

**2.4.** Vikao vya pamoja kati ya wanandarasi na Halmashauri na kuwakumbusha wajibu wao kulingana na mikataba.

Nawasilisha.

**Boaz Pius**
**MHANDISI WA MAJI (W)**
**KWIMBA.**

## 2.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI IDARA USAFI NA MAZINGIRA

| Na | Mpango Kazi/Shughuli | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Kuratibu kwa kushirikiana na Kitengo cha Afya – Kinga katika kampeni ya usafi wa Mazingira kwa kila jumamosi ya mwisho wa Mwezi | ➢ Kampeni ya usafi wa mazingira imefanyika katika Kata 10 ambazo ni:- (1) Nyamilama (Kijiji cha Nyamilama), (2) Mantare (Kijiji cha Ishingisha), (3) Iseni (Kijiji cha Nyashana), (4) Igongwa (Kijiji cha Manguluma), (5) Mwankulwe (Vijiji vya Mwankulwe na Ikunda), (6) Ngudu (Ngumo), (7) Lyoma (Kijiji cha Lyoma), (8) Kikubiji (Vijiji vya Kikubiji na Shilima), (9) Mhande (Kijiji cha Gulumwa) na (10) Ng'wahalanga (Kijiji cha Mahiga) |
| 2 | Kushiriki kwa pamoja na kitengo cha Misitu na Wakala wa misitu Tanzania katika kuzuia uharibifu wa mazingira wa ukataji miti holela na katika upandaji miti | ➢ Doria imefanyika ya kuzuia ukataji miti holela katika Kata za Hungumalwa, Sumve, Bungulwa, Ngula na Ngudu na katika shamba la miti la Icheja na hatua stahili zilichukuliwa<br>➢ Wakazi wanaoishi kandokando ya barabara ya Ngudu – Malemve wamehamasishwa kupanda miti ambapo jumla ya miti 6,750 ilipandwa katika maeneo hayo husika |
| 3 | Udhibiti wa taka Ngumu katika maeneo mbalimbali | ➢ Uzoaji wa taka ngumu umefanyika katika Mji wa Ngudu kwa kushirikiana na wataalam Idara ya Afya Kinga |
| 4 | Kusimamia sheria ya usimamizi wa mazingira katika utekelezaji wa miradi mbalimbali | ➢ Mradi unaotarajiwa kujengwa wa Kituo cha mafuta cha Sumve umefanyiwa tathmini ya athari ya Mazingira na taarifa kuwasilishwa Baraza la hifadhi ya Mazingira |
| 5 | Zoezi la ukaguzi wa Vyeti kwa watumishi wa Umma | ➢ Watumishi wote wa idara wamehakikiwa vyeti vyao husika |
| 6 | Kuandaa taarifa mbalimbali zinazohusina na usafi na Mazingira | ➢ Taarifa ya tatu ya hali ya Mazingira ya Wilaya ya Kwimba iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Katibu Tawala Mkoa kwa ajili ya kuunganishwa na kutoa taarifa ya tatu ya hali ya Mazingira nchini<br>➢ Taarifa za Usafi wa kila jumamosi ya mwisho wa mwezi ziliandaliwa na kuwasilishwa Mkoani kwa ajili ya kupelekwa TAMISEMI |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Kutoa elimu ya uhifadhi wa Mazingira | ➢ Elimu imetolewa kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari Ngudu wanaoandaa maandiko miradi yanayohusiana na utunzaji wa mazingira |

**CHANGAMOTO**

- Uhaba wa watumishi katika idara husika katika ngazi ya Wilaya na Kata
- Uhaba wa vitendea kazi
- Kutofika kwa wakati rasilimali fedha kulingana na bajeti iliyopitishwa hivyo kupelekea utendaji kazi kutofanyika kwa wakati uliokusudiwa

**MIKAKATI**

- Kuendelea kuwatumia ipasavyo wataalamu wa Afya waliopo hadi katika ngazi ya Kata
- Kushirikiana na Idara ya nyingine katika kutumia rasilimali zilizopo katika kukabiliana na upungufu wa vitendea kazi
- Kuendelea kutumia zaidi mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya katika kutekeleza Kazi zilizopo

Naomba kuwasilisha,

Deogratias J. Makungu
Afisa Usafishaji na Mazingira Wilaya
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

## 3.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KITENGO CHA SHERIA ROBO YA NNE

### 1.0 Watumishi katika Kitengo:

Kitengo cha Sheria kwa sasa kina jumla ya Watumishi wenye taaluma ya Sheria watatu. Kati ya hao, mmoja ni Mkuu wa Kitengo na wengine ni Wanasheria wa kawaida. Kitengo pia kinaye Mhudumu mmoja ambaye anatumiwa kwa ushirikiano na Idara nyingine

### 2.0 Shughuli za Kitengo

Kitengo kimekuwa kinasimamia na kutekeleza shughuli mbali mbali za kisheria. Shughuli hizo ni pamoja na; kusimamia mashauri mbali mbali yanayoihusu Halmashauri yaliyopo Mahakamani, kusimamia utekelezwaji wa Sheria, kuandaa na kupitia nyaraka mbali mbali za kisheria zinazohusiana na mashauri mapya na yanayoendelea Mahakamani; kuandaa

nyaraka mbali mbali za kisheria zinazohusiana na mikataba; kuandaa rasimu za Sheria Ndogo za Halmashauri; kushughulikia taarifa za madai (demand notes), kuratibu shughuli za uendeshaji wa Mabaraza ya Kata, kuhudhuria kwenye vikao vya Kamati za kudumu za Halmashauri; kutoa ushauri wa kisheria kwa Halmashauri na Idara zake.

**3.0 Mashauri yaliyopo Mahakamani**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imekuwa na jumla ya mashauri ya madai nane (8) Mahakamani yanayosimamiwa na Kitengo cha Sheria. Katika mashauri yote hayo Halmashauri ndiyo inayoshtakiwa. Kati ya mashauri hayo, mashauri sita bado yanaendelea na mawili yaliweza kumalizika ambapo moja Halmashauri ilishinda na jingine liliondolewa Mahakamani kwa makubaliano ya wahusika baada ya Halmashauri kulipa deni nje ya Mahakama. Taarifa ya kina ya mashauri hayo pamoja na maendeleo yake na Mahakama yaliyomo ni kama inavyoonekana kwenye kwenye **Jedwali "A".** Aidha, kwa upande mwingne Halmashauri inayo mashauri mengine nane (8) yaliyopo katika Mahakama za Mwanzo yanayoendeshwa na Idara ya Fedha. Hii ni kwa sababu kwa mujibu wa Sheria Wanasheria hawaruhusiwi kuwawakilisha wadaawa katika Mahakama za Mwanzo. Hata hivyo Kitengo kimekuwa kikihusika katika kutoa maelekezo na kufuatilia mwenendo wake. Mashauri hayo yanahusu Mawakala mbali mbali wa Halmashauri ambao muda wa mikataba yao ilimalizika wakiwa na madeni. Orodha ya mashauri hayo ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali "B".**

**4.0 Mabaraza ya Kata**

Halmashauri ina jumla Mabaraza ya Kata 30 hai yaliyomo kwenye Kata 30 za Halmashauri. Jukumu kubwa la vyombo hivi ni kutatua migogoro kwa haraka zaidi, gharama nafuu na kwa ufanisi zaidi. Moja ya mafanikio yaliyofikiwa na Mabaraza haya ni kutatua migogoro mingi kwa haraka zaidi ikilinganishwa na Mahakama za kawaida. Matatizo makubwa yanayoathiri utendaji wa Mabaraza haya ni pamoja na kutopata mafunzo kuhusiana na utendaji wao wa kazi kutokana na kukosekana kwa bajeti. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 Kitengo cha Sheria kilikuwa kinashughulikia mchakato wa kuhuisha Mabaraza haya kwa kuratibu uchaguzi wa wajumbe wapya, na kuthibitisha majina ya wajumbe kupitia vikao vya Halmashauri ambapo wajumbe wa Mabaraza yote tayari wamethibitishwa.

**5.0 Sheria Ndogo:**

Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 Kitengo cha Sheria kilikuwa kinashughulika na mchakato wa utungaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba (Kodi ya Majengo) za mwaka 2016. Rasimu hii tayari imewasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa pamoja na TAMISEMI kwa ajili ya kuidhinishwa kabla ya kuanza kutumika rasmi. Katika mwaka mpya wa fedha Kitengo kinatarajia kushirikiana na Idara za Halmashauri kwa ajili ya kuhuisha Sheria Ndogo zilizopo ili ziweze kwenda na wakati.

**6.0 Changamoto**

Changamoto kubwa zinazokikabili Kitengo cha Sheria ni upungufu wa rasilimali fedha kwa ajili ya kununulia vitabu vya Sheria, magazeti ya Serikali, shajala, mafuta, wino wa printa na gharama kuwezesha kuhudhuria katika Mahakama mbali mbali na kukagua shughuli za Mabaraza ya Kata na Vijiji.

Naomba kuwasilisha.

Stamili A. Ndaro
**Mkuu wa Kitengo cha Sheria**
**H/W – KWIMBA**

**4.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI IDARA YA MAENDELEO YA JAMII ROBO YA NNE.**

| Na. | Shughuli | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 1 | Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vikundi 2 vya vijana kabla ya kupatiwamikopo. | Mafunzo ya ujasiriamali yalitolewa kwa vikundi 2 vya vijana kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuendesha miradi yao kabla ya kupatiwa mkopo vyenye wanachama 88. |
| 2 | Kutoa mikopo kwa vikundi 2 vya vijana kupitia mfuko wa Maendeleo ya vijana ( YDF). | Vikundi 2 vilipatiwa mkopo wa jumla ya **Tshs.5,821,000 /=**<br>• Umoja wa Waendesha Pikipiki **Tshs.5,000,000/=**<br>• Umoja wa Maendeleo ya Vijana **Tshs. 821,000/=** |
| 3 | Kufuatilia marejesho ya mikopo kwa vikundi 14 vya wanawake na 14 vya vijana vilivyopata mikopo toka mfuko wa | Ufuatiliaji marejesho ya mikopo kwa vikundi 14 vya wanawake na 14 vya vijana vilivyopata mikopo toka mfuko wa wanawake (WDF) na vijana (YDF |

| | | |
|---|---|---|
| | wanawake (WDF) na vijana (YDF).2015/2016 na 2016/2017 | umefanyika na jumla ya **Tsh.17, 269,450/=** zimerudishwa.<br>• Vijana **Tshs.10,530,000/=**<br>• Wanawake **Tshs.6,739,000/=** |
| 4 | Kusimamia usajili wa vikundi vya kijamii (CBO) vilivyoomba kusajili katika ngazi ya Wilaya | Vikundi vya kijamii (CBO) 852 vimetambuliwa katika ngazi ya Wilaya na jumla ya **Tshs.8, 625,000 /=** zimepatikana katika usajili huo. |
| 5 | Uundaji wa SACCO's za vijana. | Uimarishaji wa SACCOS ya Jitambue Vijana SACCOS LTD ya Sumve iliyoanzishwa na Vijana wa Kata ya Sumve na imesajiliwa Kwa Namba MZR.1998 yenye wanachama 24 na mtaji wao ni **Tshs.8,050,000/=** |
| 6 | Kushiriki katika zoezi la kugawa fedha kwa kaya maskini katika vijiji 20 | Watumishi wa idara 5 walishiriki katika ugawaji wa fedha kwa kaya maskini katika vijiji vya Mwamajila, Kikubiji, Nyamatala, Ilula, Ndamhi, Nkungulu, Nyashana, Nyamigamba, Talaga, Ishingisha na Mwamakoye, Kikubiji, Mwabaraturu, Mhulya, Ikunda, Mhalo, Shilanona, Nyamilama, Sangu na Mwagingi |
| *7* | Kutoa mafunzo ya usimamzi na uendeshaji wa miradi ya maji kwa kamati za maji 3 kwa vijiji vya Nyang'honge, Shushi , Ilula na Manayi **.** | Mafunzo yamefanyaka kwa wajumbe 36 wa kamati za maji na viongozi 7 wa vijiji na kata kuhusu usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji ngazi ya kijiji. |
| *8* | Kushiriki katika vikao vya kisheria vya Halmashauri. | Idara ilishiriki katika vikao vya CMT, Uchumi Ujenzi na Mazingira na kikao cha fedha, uongozi na mipango |
| *9.* | Kutoa fedha za lishe kwa vikundi 84 vya Waishio na VVU na UKIMWI. | Jumla ya vikundi 62 kati 84 vya Watu Waishio na VVU na UKIMWI vimepatiwa kiasi cha **TSh. 15,038,286/-** kwa ajili ya lishe na kuendeleza miradi ya kuongeza kipato. |
| *10.* | Kufanya vikao vya kamati ya kudhibiti UKIMWI Wilaya (CMAC) kuhusu kujadili taarifa za utekelezaji robo ya I,II,na III, 2016/2017. | Vikao vya kamati ya kudhibiti UKIMWI Wilaya (CMAC) Vimefanyika kwa kuzingatia ratiba ya vikao vya Halmashauri na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji robo ya I,II na III 2016/2017. |
| *11* | Kusambaza fomu za utekelezaji wa program ya kutathmini na kurasimisha stadi za kazi zilizopatikana nje ya mfumo | Fomu zimesambazwa katika Kata 30. Kata 13 kati ya 30 zimerejesha fomu katika Ofisi ya M/Jamii na vijana 157 wamejitokeza kujaza fomu hizo na tumeziwasilisha kwenye ofisi za VETA kanda ya |

| | | |
|---|---|---|
| | rasmi wa mafunzo katika kata 30. | Mwanza. |
| *12* | Kutoa Mafunzo kwa watu maarufu na Watendaji katika Jamii kuhusu tabia hatarishi zinazohusiana na Mila na Desturi katika Jamii | Mafunzo yalitolewa kwa washiriki 37 kutoka katika Vijiji vya Shighumulo,Nyamilama, Ibindo na Mwabomba. |
| *12* | Kuratibu na kusimamia maadhimisho ya siku ya Wanawake Duniani katika Kata ya Ngudu. | Maadhimisho yalifanyika kwa shughuli zifuatazo kufanyika<br>• Kupanda miti100 katika Kitongoji cha Mwagimagi na Shule ya msingi Budula.<br>• Mdahalo kwa washiriki juu ya changamoto zinazoweza kuwa kikwazo katika mchakato wa wanawake katika Uchumi wa Maendeleo ya Viwanda.<br>• Maonesho ya bidhaa za Vikundi vya Wanawake siku ya maadhimisho uwanjani |
| *13* | Uhakiki wa vikundi vilivyoomba kusajiliwa 852. | Ufuatiliaji umefanyika kwa vikundi 413 kwenye Kata 13 kati ya 30 kwa lengo la kuhakiki miradi yao ya kiuchumi Kikubiji,Nkalalo,Bupamwa,Mwankulwe,Nyambiti,Fukalo,Mwamala,Ngulla,Hungumalwa,Ng'hundi,Sumve, Nyamilama na Maligisu uhakiki unaendelea kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Kata zilizobaki. |
| *14* | Kushiriki katika mikutano ya hadhara katika Vijiji vya ,Kikubiji,Maligisu, ,Malya,Mwabilanda Ngulla na Izizimba A' | Mikutano ya Hadhara ilifanyika katika vijiji 6 juu ya Afya ya Jamii ikisisitiza zaidi juu ya Uzazi wa Mpango kwa lengo la kupunguza vifo vya mama na mtoto. |
| *15* | Kufuatilia Wahudumu wa wagonjwa wa majumbani kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Red Cross (Mwanza). | ufatiliaji ulifanyika kwa Red Cross kutoa Vifaa vya kusaidia vikundi vya WAVIU na HISA .Pia vituo na zahanati vilitembelewa ambayo ni Malya,Nyambiti , Mwampulu, Buyogo na Hospital ya Sumve |

**CHANGAMOTO**

- Vikundi vinahitaji mafunzo ya mara kwa mara ili kuwawezesha kuendesha shughuli zao kwa tija na ufanisi.
- Ukosefu wa vitendea kazi na kushindwa kufikia Kata zote 30 katika zoezi la uhakiki wa Miradi ya vikundi vya kiuchumi.
- Vikundi kuwa na miradi ya kiuchumi ambayo sio endelevu kwa ajili ya kuwakomboa kiuchumi.

**MAPENDEKEZO/ MAONI.**

- Idara kuendelea kuelimisha vikundi vya ujasiriamali hususani vilivyopewa mikopo ili kuviwezesha kusimamia shughuli / miradi yao kwa ufanisi
- Idara inaendelea kufuatilia marejesho ya mikopo.
- Idara ya M/Jamii kuendelea na Zoezi la kutembelea vikundi kwa kila mwezi.

Naomba kuwasilisha.

*Johnson F.Muyombya*

*Kny: Afisa Maendeleo ya Jamii na Vijana(W)*

## 5.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI ROBO YA IV KUANZIA APRILI - JUNI, 2017

Ifuatayo ni taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi robo ya Nne kuanzia Aprili - Juni, 2017.

### A. SHUGHULI ZILIZOPANGWA

| NA | SHUGHULI ILIYOPANGWA | HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Kudhibiti magonjwa ya mifugo kwa kuogesha mifugo kutumia majosho na kunyunyiza kwa pampu za mkono mahali ambapo hakuna huduma ya josho, chanjo na kunywesha mifugo dawa ya kuangamiza minyoo | Uogeshaji wa mifugo ulifanyika katika majosho 3. katika kipindi hicho jumla ya michovyo 11,067 ilifanyika kama ifuatavyo; Ng'ombe (10,619), Mbuzi (1,499), Kondoo (697) na Mbwa (45). Aidha jumla ya ng'ombe 33,279, mbuzi 11,253 na kondoo 4,624 walinyunyuziwa dawa kwa kutumia pampu za mkono.<br>Jumla ya kuku 5,358 walipata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa Kideri katika Kata ya Shilembo<br>Kwa robo hii, Jumla ya ng'ombe 11,189 na mbuzi/kondoo 5,529 walipatiwa dawa za kuangamiza minyoo |
| 2 | Kutibu magonjwa ya mifugo yaliyojitokeza | Ng'ombe 450 waliugua na kutibiwa kati ya hao 384 walipona na 65 walikufa kutokana na magonjwa yafuatayo; Ndigana kali (182), ndigana baridi (147), Babesiosis (71) na Heart water (50)] |
| 3 | kufanya ukaguzi wa nyama na kusimamia usafi katika machinjio zilizopo ili kuweza kukidhi ubora na usalama wa afya ya walaji | Ukaguzi na usimamizi wa usafi wa nyama ulifanyika katika machinjio ya Ngudu, na machinjio ndogo za Sumve, Malya, Hungumalwa na Nyambiti. Jumla ya ng'ombe 461, mbuzi 1,469, kondoo 444 na nguruwe 23 walichinjwa na kukaguliwa. |
| 4 | Kusimamia shughuli za biashara ya mifugo minadani | Jumla ya ng'ombe 5,566, mbuzi 1,581 na kondoo 766 walinunuliwa, wakachunguzwa afya zao na vibali vikatolewa kwa ajili ya kusafirishia sehemu mbalimbali ndani na nje ya wilaya. |
| 5 | Kufanya ukaguzi wa samaki na mazao ya samaki | Ukaguzi wa samaki na mazao yatokanayo na samaki ulifanyika katika masoko na magulio ambamo samaki huingizwa kwa lengo la ki-biashara. Katika kipindi hicho hapakuwepo na samaki walioonekana kuvuliwa kwa njia haramu. |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Utambuzi na usajili wa mifugo | Katika Kata za Ngudu, Igongwa, Ng'hundi, Mwang'halanga, Nyamilama, Bungulwa, Hungumalwa na Malya, mikutano kwa ajili ya kuhamasisha wafugaji kuhusu zoezi la upigaji chapa ng'ombe imeendelea kufanyika.<br>Zoezi la upigaji chapa ng'ombe linatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2017 baada ua utayarishaji wa vyuma vya kupigia chapa na vifaa vingine kukamilika. |
| 7 | Kushiriki sherehe za Maadhimisho ya wiki ya maziwa mwaka 2017 Kitaifa, Mkoani Kagera ambapo Kilele cha maadhimisho hayo ni Tarehe 01/06/2017 | Maadhimisho ya wiki ya maziwa wilayani mwaka 2017 chini ya Kaulimbiu "Kunywa Maziwa, Jenga Afya, Furahia Maisha" yalifanyika mjini Ngudu tarehe 31/5/2017 na 01/6/2017 yakishirikisha wadau mbalimbali wa maziwa wakiwemo; Viongozi, Wataalam wa Kilimo/Mifugo, Wazalishaji, Wasindikaji, Wauzaji na Watumiaji wa maziwa |

**B. CHANGAMOTO**

- Ukosefu wa maji katika baadhi ya majosho kulisababisha shughuli za uogeshaji kusimama
- Ukosefu/uchakavu wa uzio katika minada kulisababisha baadhi ya wafanya biashara kutorosha mifugo yao na kupelekea kukwepa kutoa ushuru
- Upungufu wa wataalam wa Mifugo na Uvuvi kuna sababisha shughuli za ugani kushindwa kufika katika maeneo mengine ya wilaya
- Baadhi ya wafugaji kuchelewa kutoa taarifa kwa wataalam wa mifugo pindi mifugo yao inapougua hali inayosababisha vifo vya mifugo.
- Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendesha zoezi la Upigaji chapa mifugo na kufanya ufuatilia wa shughuli za ugani vijijini

**C. MIKAKATI**

1. Kuendelea kuingiza katika Mpango na bajeti shughuli za Ujenzi/Ukarabati wa miundombinu ya mifugo kama kujenga visima virefu maeneo ya majosho na uzio
2. Kuendelea kuiomba Serikali kutoa nafasi za ajira mpya za wataalam wa mifugo na uvuvi

3. Kuendelea kutoa ushauri kwa wafugaji kuhusu ufugaji bora na kuwataka pale mifugo yao inapoonekana na dalili ya kuugua watowe taarifa haraka kwa wataalamu walioko katika maeneo yao ili matibabu yaanze kwa wakati.
4. Kuendelea kuhamasisha wafugaji kuhusu umuhimu na faida za upigaji chapa mifugo yao na kuchangia gharama za zoezi hilo.

Mahega D. Mahega
KAIMU AFISA MIFUGO NA UVUVI (W)
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

## 6.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KAZI KWA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA KWA KIPINDI CHA JULAI 2016 – JUNI, 2017

| NA | LENGO | UTEKELEZAJI | MAELEZO/MIKAKATI |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuhakikisha Vikao vyote vya Kisheria vinafanyika vikiwepo Vikao vya Idara. | • Vikao vyote vimefanyika kwa mujibu wa ratiba ilivyokuwa imepangwa, kuwepo kwa Mihtasari ya Vikao.<br>• Aidha Vikao vya Watumishi wote wa Makao Makuu ya Halmashauri vimefanyika. | Idara inaendelea kusimamia Vikao kwa mujibu wa ratiba. |
| 2 | Kuhamisha na kurekebisha taarifa ya watumishi katika mfumo wa mishahara (LAWSON – HCMIS). | • Watumishi wote waliohama, kustaafu, kuacha kazi na kufariki waliondolewa kwenye mfumo wa mishahara (Lawson)<br>• Aidha watumishi (Walimu) waliopandishwa vyeo walirekebishiwa mishahara yao. | Zoezi linaendelea |
| 3 | Kuandaa, kuwasilisha na kusimamia Bajeti ya Mishahara Machi 2017 (PE Budget). | • Uwepo wa taarifa ya Budget kutoka kwenye mfumo wa Mishahara 2017/2018. Uwepo wa Kitabu cha bajeti 2017/2018. | Kitabu kiliandaliwa na kuwasilishwa sehe mu husika. |
| 4 | Kusimamia utendaji kazi kwa WEO's na VEO's na wataalam waliopo kwenye kata kuhakikisha wanakuwepo kwenye vituo vya kazi. | • Kuwaandikia barua za kuwataka wawepo vituoni.<br>• Kufanya kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu za Utumishi<br>• Kuhimiza ukusanyaji wa mapato na kuwasilisha kwa wakati. | Zoezi ni endelevu. Aidha watendaji wote wameandikiwa barua kumb Na. MZA/KDC/R.30 VOL V/4/151 ya tarehe 10/01/2017 kuwataka wawepo vituoni. |
| 5 | Kuandaa na kuhakikisha TANGE (seniority list) ya Watumishi ipo wakati wote, Ikama ya Watumishi kuwepo wakati wote na inarekebishwa kulingana na mahitaji ya Watumishi. | • kuwepo kwa TANGE ya Halmashauri<br>• Kuwepo kwa Ikama ya Watumishi kwa Halmashauri. | Kazi hii ni endelevu |
| 6 | Kupokea na kutuma taarifa mbalimbali | • Idara imeshiriki vizuri kupokea taarifa na maagizo mbalimbali kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, Mkoa na Wizara yalipokelewa | Taarifa zitaendelea kutumwa /kufanyiwa kazi kadri zinavyowasilishwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kufanyiwa kazi na kutumwa kadri yalivyohitajika. | |
| 7 | Kupokea na kuwapangia wanachuo sehemu za kufanyia mazoezi kwa vitendo. | • Wanachuo kutoka vyuo mbalimbali walipokelewa na kupangiwa sehemu/Idara za kufanyia mafunzo kwa vitendo kulingana na fani wanazosomea. | Zoezi ni endelevu wanachuo wataendelea kupangiwa kulingana na wanavyowasilisha maombi na uwepo wa nafasi za za kufanya mafunzo kwa vitendo. |
| 8 | Kusimamia zoezi la ujazaji na tathimini ya fomu za upimaji utendaji kazi-OPRAS. | • Zoezi limesimamiwa lakini kuna msukumo mdogo kutoka kwenye Idara, hivyo kuchelewesha zoezi la ujazaji na upimaji,tathimini/mapitio ya nusu mwaka. | Kila Idara iweke msisitizo na maelekezo kwa watumishi wake |
| 9 | Kusimamia na kufanya Uhakiki wa Vyeti vya Watumishi | • Idara ilisimamia vyema na kwa umakini zoezi hili na matokeo ni kama ifuatavyo;<br>1. Watumishi 36 wameagundulika wana Vyeti feki wamefutwa Payroll.<br>2. Watumishi 46 wana Vyeti pungufu na wanaendelea kupata Mishahara hadi taarifa nyinginezo zitakapotolewa na Baraza la Mitihani.<br>3. Watumishi 5 waliotuhumiwa kuwa na Vyeti feki wamerejeshwa Payroll baada ya kuthibitika Vyeti vyao havina mapungufu. | Zoezi hili bado linaendelea na taarifa itaendelea kutolewa. |
| 10 | Kushughulikia masuala ya kinidhamu. | • Idara inaendelea kuwachukulia hatua watumishi kwa kufuata sheria na kanuni za Utumishi kadri inavyojitokeza. | Kazi hii ni endelevu |
| 1<br>11 | Kufuatilia kibali cha vibali vya ajira kutoka menejimenti ya Utumishi na kutuma maombi ya vibali vya Ajira 2016/2017. | Vibali vimeombwa sekretarieti ya ajira Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kutumwa tarehe 07/12/2016. | Majibu yanasubiriwa kujua jumla na aina ya nafasi tulizo kubaliwa. |
| 12 | Kuandaa takwimu za wastaafu Julai 2016 hadi Juni, 2017. | Takwimu ziliandaliwa kupitia mfumo wa LAWSON kwa watumishi wanaotarajia kustaafu kuanzia Julai 2016 hadi Juni, 2017. kama ifuatavyo:-<br>-Elimu Msingi – 38<br>-Elimu Sekondari -1<br>-Afya -1 na Utawala 3 jumla 43 | Kazi hii ni endelevu ili kuweza kudhibiti kutokuwepo kwa watumishi hewa. |
| 13 | Kuratibu zoezi la wanufaika wa mikopo ya Elimu ya juu. | Jumla ya wanufaika 44 wameratibiwa na taarifa zao zimeingizwa kwenye mfumo wa mishahara tayari kuanza makato kurejesha fedha za serikali. | Zoezi linaendelea |
| | Kuratibu shughuli za Tume maalum ya Mkuu wa Mkoa | Idara iliratibu vyema shughuli za Tume maalum ya Mkuu wa Mkoa iliyofa kazi yake | Idara itaendelea kuipa Ushirikiano Tume yoyote |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14 | katika Halmashauri yetu. | kwa siku 14 kuanzia tarehe 13/03/2017. | itakayoteuliwa kufanya kazi katika Halmashauri yetu. |
| 15 | Kutoa Mafunzo ya kuboresha Utendaji kazi kwa VEOs, WEOs, Maafisa Ugani na Wahe. Madiwani | Mafunzo yalitolewa kuwajengea uwezo Watumishi tajwa na Wahe. Madiwani. | Mafunzo ya aina hii yataendelea kutolewa kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu. |
| 16 | Kusimamia zoezi la Uhakiki wa madeni ya Watumishi -Walimu yasiyo ya Mishahara. | Idara ilisimamia vyema zoezi hili kwa pamoja na Timu ya Mkoa, TSC, CWT, Elimu Msingi na Elimu Sekondari. | Idara itaendelea kusimamia mazoezi mengine kadri yatakavyojitokeza. |
| 17 | Kuratibu na kusimamia kazi ya Ukaguzi wa Rasilimali watu na uzingatiaji taratibu, Sheria na Kanuni katika utoaji huduma. | Idara iliratibu na kusimamia Ukaguzi huo uliofanywa na Timu ya Maafisa toka Tume ya Utumishi wa Umma. | Idara itazingatia maelekezo yote yaliyotolewa na Tume hiyo kwa ajili ya kuboresha huduma kwa Watumishi. |

**A I: HALI HALISI YA WATUMISHI - KIIDARA**

| Na | Idara | Kasma Ndogo | Mahitaji | Waliopo | Upungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Utumishi na Utawala | 5004 | 294 | 129 | 47 |
| 2 | Elimu Sekondari | 5008 | 1081 | 858 | 223 |
| 3 | Elimu Msingi | 5007 | 2221 | 1704 | 517 |
| 4 | Mifugo na Uvuvi | 5034 | 76 | 36 | 40 |
| 5 | Ujenzi | 5014 | 32 | 27 | 5 |
| 6 | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 5033 | 108 | 46 | 62 |
| 9 | Afya | (5010,5011,5012,5013) | 665 | 400 | 265 |
| 10 | Maji | 5017 | 29 | 27 | 7 |
| 11 | Watendaji wa Kata/Vijiji | 5031 | 149 | 143 | 6 |
| 12 | Elimu Utawala | 5006 | 11 | 11 | 0 |
| | **JUMLA** | | **4666** | **3381** | **1172** |

**B II HALI YA WATUMISHI**

| Na | Idara | Jumla | Walio Masomoni | Wastaafu | Kuacha Kazi | Kifo | Utoro |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Utumishi na Utawala, VEO's,WEO's | 272 | 8 | 3 | 0 | 0 | 2 |
| 2 | Elimu Msingi na Elimu Utawala | 1715 | 51 | 38 | - | 8 | 6 |
| 3 | Elimu Sekondari | 858 | 118 | 1- | - | 1 | 2 |
| 4 | Afya | 398 | 17 | 1 | - | 2 | 7 |
| 5 | Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika | 46 | 4 | 0 | - | - | - |
| 6 | Mifugo na Uvuvi | 36 | 1 | 1 | - | - | - |
| 7 | Maji | - | - | - | - | - | - |
| | **JUMLA** | **3325** | **199** | **44** | **Hakuna** | **11** | **17** |

**C III AJIRA MPYA**

| Na | Idara | Cheo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Elimu Sekondari | Walimu | 21 |
| 2 | Afya | Madaktari | 2 |
| | **JUMLA** | | **23** |

**III: CHANGAMOTO**:

- Idara inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Ofisi za Watendaji wa Kata na Vijiji.
- Ukosefu wa vyombo vya usafiri kwa Watendaji wa Kata na Vijiji.
- Ukosefu wa fedha za kuendeshea Idara na kupelekea kukosa nyenzo muhimu kama mafuta, kuwezesha ukaguzi wa Watumishi na Vituo vya kazi vilivyo nje.
- Baadhi ya Watumishi kutokaa ofisini kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
- Utoro kwa baadhi ya Watumishi hususani walioko Vijijini.

**IV: MIKAKATI:**

- Kuhamasisha ujenzi wa Ofisi za Kata na Vijiji kupitia Kamati za Maendeleo za Kata (WDC).
- Kutayarisha andiko ili kupata Mfadhili wa kuwakopesha Watendaji vyombo vya Usafiri kwa bei nafuu
- Kufanya ukaguzi na ziara ya mara kwa mara kwenye vituo vya kazi hususani vilivyoko Vjijini na kuchukua hatua kwa Watumishi wazembe.
- Kushirikiana na Wakuu wa Idara/Vitengo kupata taarifa za kila Mwezi zinazoonesha Watumishi waliofariki, Staafu, Acha kazi na Watumishi watoro, ambao hawapo v6ituoni bila taarifa yoyote toka kwa Mwajiri.
- Kushirikiana na Waratibu Elimu Kata na Wakuu wa Shule kusimamia na kutoa taarifa kila Mwezi kutoka Mashuleni ili kudhibiti uwepo wa Watumishi watoro na kuweza kuchukuliwa hatua stahiki ikiwemo ya kuondolewa kwenye malipo ya Mishahara.

Naomba kuwasilisha.

Cornel, E.
**KAIMU MKUU WA IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI,**
**HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.**

## 7.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA ELIMU SEKONDARI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (APRILI - JUNI, 2017).

| S/N | ENEO/SWALA | HALI YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Kuingiza Takwimu za Shule za Sekondari 2017 kwenye mfumo wa BEMIS, TAMISEMI, | Kazi ilifanyika na kukamilika. |
| 2 | Kufanya maandalizi ya awali ya uendeshaji wa Mtihani wa Taifa wa kidato cha VI, 2017. | Maandalizi yalikamilika na mtihani ulifanyika vizuri bila dosari yoyote. |
| | Kusimamia uendeshaji wa Mtihani wa Kidato cha V 2017. | Mtihani ulikamilika bila dosari yoyote. |
| 3 | Kufuatilia hali ya ufundishaji shuleni | Kazi ya ufuatiliaji ufundishaji ilifanyika kwa kushirikiana na Idara ya Elimu Msingi. |
| 4 | Kuandika taarifa za Robo ya tatu, 2016/2017 | Taarifa zote zilizotakiwa kuandikwa ziliandikwa na |

| | | |
|---|---|---|
| | | kuwasilishwa kunakotakiwa vizuri. |
| 5 | Kusimamia ujenzi wa miundombinu katika Shule ya Sekondari Bupamwa chini ya mradi wa P4R. | Usimamizi wa mradi huu unaendelea. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni upauaji wa vyumba vya madarasavinne na ofisi, na matundu 10 ya choo yamefunikwa. |
| 6 | Kusimamia uendeshaji wa michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA. | Idara ilishiriki kikamilifu uendeshaji wa michezo hii kuanzia ngazi za shule hadi taifa. |

Naomba kuwasilisha.

## 8.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARAYA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA KUANZIA APRILI – JUNI 2017.

| Na | SHUGHULI ZILIZOPANGWA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Usambazaji wa majina ya wakulima waliokopa viuadudu vya pamba kwa maafisa watendaji wa kata. | Zoezi limefanyika na linaendelea kwa maeneo yote |
| 2 | Kufuatilia mauzo ya mbegu za mtama katika kata zote za wilaya. | Kilo 6,866 sawa na tani 6.866 zimeshachukuliwa na wakulima<br>-Kilo 162 zimetolewa bure katika kata za Ngudu, Walla, Mwagi na Mwandu |
| 3 | Kuratibu zoezi la kusambaza mahindi ya kupunguza makali ya bei tani 300 | Zoezi limekamilika la kupokea mahindi kutoka ghala la kuhifadhi Shinyanga na yamepokelewa Wilayani |
| 4 | Kufuatilia ufunguaji wa vituo vya kununua pamba | Vituo vimefunguliwa na vinanunua pamba kwa bei elekezi ya Tsh 1,200/= |
| 5 | Uhamasishaji wa vyama vya Ushirika katika kusimamia na uendeshaji wa vyama | -Wajumbe wa Bodi ya Nyambeho AMCOS (Sumve) wamehamasishwa kufanya uchaguzi wa Mwenyekiti wa mpito ili chama kipate uongozi wakati chama kinasubiria ratiba ya uchaguzi mkuu.<br><br>-Kikundi cha DAMAGI – Kimiza (Lyoma) kimehamasishwa kujiwekea akiba za mara kwa mara na kurejesha mikopo kwa wakati ili kukuza mtaji wa chama |
| 6 | Uandaaji wa sera za chama cha JITAMBUE SACCOs | Kwa kushirikiana na Bodi ya chama cha JITAMBUE SACCOS kitengo kimewashauri waandae sera ya akiba na mikopo kulingana na sheria Na.6 inavyoelekeza ya vyama vya ushirika ya mwaka 2013. |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Kusimamia vyama vya Ushirika kuandaa makisio ya mapato na matumizi. | Makisio ya mapato na matumizi mwaka 2017 kwa AMCOS ya Nang'honge, Ndami na Mwagingi yameandaliwa |
| 8 | Uhamasishaji vyama vya Ushirika kuongeza idadi ya wanachama | Uhamasishaji umefanyika kwa wajumbe wa bodi ya Jitambue SACCOS (Sumve) na Kwite SACCOS (Ngudu) kuongeza idadi ya wanachama ili kukuza mtaji wa chama |
| 9 | Maandalizi ya mkutano mkuu wa chama | Kitengo kimekutana na wajumbe wa Bodi ya Kwite kufanya maandalizi ya mkutano mkuu wa chama na kuanza kwa zoezi la uchaguzi |
| 10 | Ukaguzi wa mahesabu wa vyama vya Ushirika | Ukaguzi umefanyika katika SACCOS za Bugogo (Sumve), Kwite (Ngudu) na Ngudu Vijana (Ngudu) |
| 11 | Kuandaa mpango mkakakati na mpango biashara wa SACCOS | Mpango mkakati na Mpango Biashara kwa kipindi cha mwaka 2018 - 2022 umeandaliwa kwa kushirikiana na bodi ya Kwite. |
| 12 | Uhakiki wa vyama vya Ushirika SACCOS na AMCOS | Kitengo kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika jumla ya vyama 111 vilifikiwa kwa lengo la kubaini vyama hai na vilivyo sinzia. |

**Changamoto**

1. Ubovu wa gari la Idara ya Kilimo
2. Watendaji wa kata/vijiji kucheleweshа kuwasilisha fedha za mauzo ya mbegu za mtama
3. Wanunuzi (wasambazaji) wa mahindi kuchukua muda mrefu kulipa fedha za kununua mahindi ya kupungua makali ya bei.
4. Kampuni ya ICK inasuasua kufungua vituo, pia baadhi ya vituo vyake kupungukiwa fedha za kununua pamba
5. Wanachama kutojiwekea akiba mara kwa mara na kutorejesha mikopo kwa wakati
6. Uelewa mdogo wa sera mbalimbali za vyama vya ushirika kwa viongozi wa Bodi
7. Urejeshwaji mdogo wa madeni ya pembejeo za pamba (mbegu na viuadudu)

**Mikakati**

1. Kutengeneza gari kwa ajili ya kuratibu shughuli za kilimo
2. Kuendelea kuhimiza watendaji wote kurejesha fedha za mauzo ya mtama na kurudisha mbegu za mtama zilizobaki.
3. Kuendelea kuhimiza kampuni ya ICK Cotton kufungua vituo vyake vya kununua pamba
4. Wanachama wa kikundi kuendelea kuelimishwa kujiwekea akiba mara kwa mara na kurejesha mikopo kwa wakti kukuza mtaji na kuweza kukopeshana
5. Kuhamasisha wakulima kurejesha madeni ya pembejeo (mbegu na viuadudu)

Naomba kuwasilisha,

Eng. Magreth Kavalo

**AFISA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA (W)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA**

**9.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII – TASAF III KIPINDI CHA ROBO YA NNE (Aprili - Juni 2017)**

Naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Kitengo cha TASAF kwa kipindi cha Aprili - Juni 2017. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha na matumizi yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umeambatanishwa .

| Na | SHUGHULI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Kufanya malipo kwa Walengwa wa Mpango wa kunusuru kaya Maskini. | Kwa kipindi cha robo ya nne (Aprili - Juni 2017),kitengo kilisimamia dirisha moja la malipo kwa walengwa wa kaya maskini Mei/Juni 2017 kama ifuatavyo:<br>1. Vijiji vilivyo katika mpango ni 86.<br>2. Jumla ya fedha zilizopokelewa kutoka TASAF Makao Makuu kwa ajili ya malipo ya Aprili - Juni 2017 ni Tshs. 360,142,990.00<br>• Fedha za kulipa walengwa pekee kwa Mei/Juni 2017 zilikuwa Tshs. 332,564,000.00 ambapo jumla ya Tshs. 328,924,000.00 zililipwa kwa kaya 9,176. Kaya 87 hazikulipwa kutokana na sababu mbalimbali na fedha Tshs. 3,640,000.00 zilirejeshwa Makao Makuu kama utaratibu unavyoelekeza.<br>3. Fedha kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya, 1.5% ya vijiji na 1% ya kata kwa robo yote ni kama ifuatavyo:<br>• Halmashauri ya Wilaya (8.5%) - Tshs. 17,688,990.00<br>• Asilimia ya vijiji (1.5%) - Tshs. 8,600,000.00<br>• Asilimia ya kata (1%) - Tshs. 1,290,000.00 |
| 3 | Kuandaa taarifa. | Kitengo kiliandaa taarifa mbalimbali utekelezaji za wiki, mwezi, robo, taarifa za malipo na kuziwasilisha maeneo mbalimbali zilikohitajika (Vikao vya Halmashauri, TASAF Makao makuu, Mkoani, Katibu Tawala (W). |
| 4 | Kuhudhuria vikao | Kitengo cha TASAF kilishiriki vikao mbalimbali vya kiutawala kwa kipindi cha Aprili - Juni 2017. |

**Changamoto za utekelezaji wa shughuli;**

- Kubadilika kwa ukokotozi wa fedha kumepelekea kuwepo kwa changamoto mbalimbali ikiwemo gari kushindwa kufanyiwa matengenezo, kushindwa kutengeneza photocopy mashine, kukosekana mafuta ya ufuatiliaji.
- Wananchi kutofika kuchukua fedha zao wakati wa dirisha la malipo hivyo kulazimika kurejesha fedha hizoTASAF makao makuu.
- Wananchi katika baadhi ya vijiji kuhamahama kwa muda mfupi nabaadae kurejea tena katika vijiji vyao vya awali. Hali hii huleta usumbufu wa kuwaombea kurejeshwa tena kwenye mpango kwani kaya isipochukua mara mbili mfululizo huondolewa kwenye mfumo.

Naomba kuwasilisha,

Barnabas Kulwa
Kaimu Mratibu TASAF (W),
**Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.**

**Nakala;**
Afisa Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji (W)

## 10.0. TAARIFA YA UTEKELEZAJI KTENGO CHA TEHAMA NA UHUSIANO ROBO YA NNE YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

Naomba kuwasilisha taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha robo ya Nne ya mwaka wa fedha 2016/2017.

| NA. | SHUGHULI PANGWA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 01. | Mfumo wa Mapato ya ndani(Local Government Collection Information System) | ▪ Point of Sale 40 zimenunuliwa kwa ajili ya ukusanyaji wa mapatp ya Ndani.<br>▪ Mafunzo kwa watendaji wa Kata na Vijiji juu ya matumizi ya vifaa vya kukusanyia mapato(PoS) yamefanyika. |
| 02. | Mfumo wa Mapato wa Afya(Government of Tanzania Hospital Management System) | ▪ Ufungaji wa mfumo Kiambo(Local Area Network System) katika Hospitali ya wilaya ya Ngudu. |
| 03. | Mfumo wa EPICOR/IFMIS | ▪ Mfumo umeboreshwa kwa kuunganishwa na mfumo wa Tanzania Interbanking System(TIS) kwa ajili ya malipo na utunzaji wa fedha za Serikali BOT. |
| 04. | Mfumo wa Lawson | ▪ Mfumo wa LAWSON umeboreshwa kwa kuunganishwa na mfumo wa Government Salary Payment Portal (GSPP/EFT) kwa ajili ya kuandaa mishahara ya watumishi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | ▪ Mfumo wa LAWSON umeunganishwa na mfumo wa NIDA kwa ajili ya utambuzi wa Taarifa za watumishi. |
| 05. | Uwekaji wa Mkongo wa Taifa. | ▪ Mkandarasi ni Kampuni ya TTCL na Mkataba wa malipo umeandaliwa(LPO),hatua iliyopo ni ufungaji wa Mkongo. |
| 06. | Utengenezaji wa Tovuti ya Halmashauri | ▪ Tovuti imetengenezwa na inapatikana kwa kiunganishio cha www.kwimbadc.go.tz |
| 07. | Mafunzo ya kujenga uwezo(Capacity Building) | ▪ Maafisa Tehama na Habari wameshiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo katika matumizi ya mifumo ya GWF,TASAF MIS,LGRCIS,PREM na SDP. |

**CHANGAMOTO**

- Kukamilisha zoezi la unganishaji na usimikaji wa Mkongo wa Taifa na mfumo wa Afya.
- Upungufu wa vifaa vya ofisi na vitendea kazi.

**MIKAKATI**

- Ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi Digital Camera,Laptop ,IT Toolkit,Blower na Network tool.
- Ukamilishaji wa usimikaji wa mfumo wa GoTHMIS na Mkongo wa Taifa.
- Ununuzi wa Samani za Ofisi.
- Kushiriki mafunzo ya kujenga uwezo(short Course).

Naomba kuwasilisha.

**WILLIAM KASUJA**
**KAIMU AFISA TEHAMA NA UHUSIANO (W)**